

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS -TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SUMBAWANGA



**TARATIBU ZA UPATIKANAJI WA LESENI YA BIASHARA, VILEO NA UENDESHAJI
WA NYUMBA ZA KULALA WAGENI**

MKURUGENZI MTENDAJI(W)
S.L.P 229,
SUMBAWANGA
SIMU; 025-2802133
FAX; 025-2800301
EMAIL ded_sba@yahoo.com

**TARATIBU ZA UPATIKANAJI WA LESENI YA BIASHARA, VILEO NA UENDESHAJI WA NYUMBA
ZA KULALA WAGENI**

NA	SHERIA	TARATIBU ZA KUOMBA LESENI YA BIASHARA
1	Leseni ya Biashara chini ya Sheria ya utoaji leseni za biashara No. 25 ya mwaka 1972 na marekebisho yake ya mwaka 2014.	<p>LESENI YA KUHUIHWA (Renewal) Mwombaji anatakiwa kujaza fomu ya maombi na kuambatanisha hati ya malipo ya kodi ya mwaka husika(BLTCC) na leseni iliyoisha muda wake.</p> <p>LESENI MPYA Mwombaji anapaswa kutekeleza yafuatayo:-</p> <ul style="list-style-type: none"> ➤ Kujaza kikamilifu fomu ya maombi (gharama ya fomu ni shilingi 1000). ➤ Kuwa na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka husika (BTCC) ➤ Kuambatanisha kivuli cha Namba ya usajili wa mlipa kodi (TIN). ➤ Kuambatanisha uthibitisho wa uraia (kivuli cha cheti cha kuzaliwa, cheti cha utaifa au cheti cha kupiga kura) ➤ Uthibitisho wa maandishi eneo la kufanyia biashara. ➤ Kama ni Kampuni ambatanisha nakala ya cheti cha usajili wa Kampuni na Memorandum and Articles of Association. ➤ Kama ni jina la biashara aambatanishe vyeti vya usajili Brela (registration Certificate na Extract from Register). ➤ Kwa mwombaji ambaye sio raia wa Tanzania aambatanishe kibali cha kuishi nchini daraja A. ➤ Kama wenye Kampuni hawaishi nchini wanawakilishwa, waambatanishe hati ya kiwakili (power of Attorney). ➤ Kwa waombaji wa biashara za Kitaalamu waambatanishe vyeti vya kuruhusiwa kufanya biashara hizo kutoka Mamlaka husika. <p>MAKOSA CHINI YA SHERIA HII NI:-</p> <p>i. Kuendesha biashara bila leseni hai na halali ya biashara.</p> <p>ii. Kushindwa kuweka leseni yake mahali pa wazi ambapo itaonekana.</p> <p>iii. Kushindwa au kukataa kutoa leseni ya biashara inapotakiwa na Afisa biashara au Afisa yeyote aliyeruhusiwa kisheria.</p> <p>iv. Kutumia leseni moja kuendesha biashara zaidi ya sehemu iliyoainishwa.</p> <p>v. Kutumia leseni ya biashara eneo tofauti na lililoonyeshwa kwenye leseni.</p> <p>vi. Kutoa maelezo ya uongo ili kupata leseni</p> <p>vii. kutolipia leseni baada ya ukaguzi kufanyika.</p> <p>MALIPO YA ADA YA LESENI Malipo yatafanyika katika ofisi za Halmashauri kwa mtasilimu(cashier) siku za kazi yaani Jumatatu hadi Ijumaa saa 2:00 asubuhi hadi saa 9:00 alasiri baada ya kukamilisha taratibu zote za kisheria kwa Afisa Biashara.</p> <p>UKAGUZI WA LESENI ZA BIASHARA Ukaguzi wa leseni za biashara utafanyika mara mbili kwa mwaka na ukaguzi huo hautahusisha ukusanyaji wa ada ukikutwa huna leseni utatozwa adhabu au kufungiwa biashara. Mfanyabiashara atalazimika kupeleka Malipo ya ada ofisi za Halmashauri kwa mtasilimu(cashier) ndipo atapata leseni.</p> <p>ADHABU Mfanyabiashara atakayetenda mojawapo ya makosa yaliyoorodheshwa hapo juu atakuwa ametenda kosa la jinai na adhabu yake ni kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini (50,000)na isiyozidi laki moja(100,000) au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.</p>

2	<p>Leseni za vileo chini ya sheria No. 68 ya mwaka 1968 na marekebisho yake ya mwaka 1981</p>	<p>Waombaji wa Zamani Mwombaji ajaze fomu ya maombi na aambatanishe leseni iliyoisha muda wake.</p> <p>Waombaji Wapya Mwombaji ajaze kikamilifu fomu ya maombi na apitishe ngazi zote zilizoonyeshwa kwenye fomu ya maombi na aambatanishe na nyaraka zifuatazo:-</p> <ul style="list-style-type: none"> ➤ Uthibitisho wa maandishi wa kuwa na eneo la kufanya biashara. ➤ Kama ni Kampuni aambatanisha nakala ya cheti cha usajili wa Kampuni na Memorandum and Articles of Association. ➤ Kama ni jina la biashara aambatanishe vyeti vya usajili Brela (registration Certificate na Extract from Register). ➤ Kwa mwombaji ambaye sio raia wa Tanzania aambatanishe kibali cha kuishi nchini daraja A. ➤ Kama wenye Kampuni hawaishi nchini wanawakilishwa waambatanishe hati ya kiwakili power of Attorney). <p>Makosa chini ya sheria hii;-</p> <p>Mfanyabiashara atakayetenda moja wapo ya makosa yaliyotajwa hapa chini atakuwa ametenda kosa la jinai na atashtakiwa na akibainika kutenda kosa hilo atalipa faini au kifungo au adhabu zote kwa pamoja.</p> <ul style="list-style-type: none"> ➤ Kuuza pombe bila leseni. ➤ Kufanya biashara eneo tofauti na lililoainishwa kwenye leseni. ➤ Kumuuza pombe mtu wa miaka chini ya kumi na sita. ➤ Kubadili eneo la kufanya biashara bila idhini ya mamlaka ya utoaji leseni za vileo. ➤ Kuendelea kumuuzia mteja aliyelewa pombe. ➤ Kuruhusu eneo la biashara kuwa danguro au la kufanyika shughuli za kamari. ➤ Kuajiri mtu chini ya miaka kumi na sita (16) kuuza pombe ➤ Kuruhusu mtu mwenye umri chini ya miaka kumi na sita kukaa eneo la kuuzia pombe. ➤ Kutoweka leseni sehemu ya wazi, ambapo itaonekana kwa urahisi na wakaguzi. ➤ Kuruhusu/kuleta fujo katika eneo la biashara ➤ Kuuza pombe muda ambao ni kinyume cha sheria ➤ Kufanya biashara ya pombe kwa kutumia leseni ya vileo ambayo haistahili. ➤ Kuuza viloba au pombe nyingine yo yote na mtu asiye na leseni halali yabiashara ya vileo. <p>MALIPO YA ADA YA VILEO Malipo yaleseni ya vileo yatafanyika katika ofisi za Halmashauri kwa Mtasilimu (cashier) baada ya kukamilisha taratibu zote kisheria kwa Afisa Biashara</p> <p>ADHABU Mfanyabiashara atakayetenda mojawapo ya makosa yaliyoordheshwa hapo juu atakuwa ametenda kosa la jinai na adhabu yake ni kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi laki moja au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.</p>
---	---	---

3	<p>Ushuru wa nyumba za kulala wageni Hotel levy act No. 23 ya mwaka 1972 na marekebisho ya sheria ya fedha namba 16 ya mwaka 2015 iliyorekebisha sheria ya fedhazaserikal i za mitaa sura 290 kifungucha 4 , sambamba na waraka wa serikali (OR-TAMISEMI wa Disemba 2015)</p>	<p>Mwombaji anapaswa kuwa na leseni ya biashara na kutekeleza yafuatayo;-</p> <ul style="list-style-type: none"> ➤ Mwombaji anapaswa kujaza fomu za marejesho (returns) kulingana na idadi ya wageni waliolala kwenye vyumba kwa mwezi . ➤ Mfanyabiashara lazima atunze register ya wageni ➤ Mfanya biashara mwenye nyumba ya kulala wageni anapaswa kulipa malipo ya asilimia kumi (10%) ya mapato ya mwezi. ➤ Mfanyabiashara anapaswa kujaza fomu zinaoonyesha idadi ya vyumba na gharama zinazotozwa kwa kila chumba. ➤ Malipo yanatakiwa kulipwa sio zaidi ya siku saba tangu mwezi umalizike. ➤ Mfanyabiashara atatakiwa kulipa faini ya asilimia ishirini na tano (25%) kwa kuchelewesha malipo na faini itaongezeka kwa asilimia kumi (10%) kwa kila mwezi atakaoendelea kuchelewesha malipo. <p>Makosa chini ya sheria hii:-</p> <p>Mfanyabiashara atakayetenda mojawapo ya makosa yaliyoorodheshwa hapo chini atakuwa ametenda kosa la jinai.</p> <ul style="list-style-type: none"> ➤ Kushindwa kulipa ushuru wa malazi anaotakiwa kulipa kwa mwezi. ➤ Kukataa kutoa taarifa zinazotakiwa kuhusiana na wageni wanaolala kwenye nyumba ya wageni. ➤ Kushindwa kutunza kumbukumbu (register) ya wageni. ➤ Kutotoa risiti kwa wageni wanaolala kwenye nyumba ya wageni. ➤ Kuzuia Maofisa wa Serikali waliorushusiwa kisheria kutekeleza wajibu wao (ukaguzi). ➤ Kushindwa kutekeleza amri (Notice) atakayopewa na mamlaka halali. ➤ Kutoa taarifa ya uongo kwenye kumbukumbu yeyote inayotumika kwa ajili ya kudanganya au kushindwa au kukataa kujibu maswali vizuri kwa Afisa wa Serikali aliyepewa madaraka na sheria hii. <p>MALIPO YA USHURU WA NYUMBA ZA KULALA WAGENI</p> <p>Malipo ya ushuru wa nyumba za kulala wageni yatafanyika kwa Mtasilimu wa Halmashauri(cashier) sio zaidi ya siku saba baada ya mwezi kuisha.</p> <p>UKAGUZI WA VITABU VYA WAGENI</p> <p>Ukaguzi wa vitabu vya wageni utafanyika wakati wo wote na Afisa Biashara au Mtendaji wa kata ili kujiridhisha kama matumizi ya vitabu yanafanyika kwa mujibu wa sheria na malipo ya kila mwezi yanafanyika.</p> <p>ADHABU</p> <p>Kwa kutenda mojawapo ya makosa haya mfanyabiashara atatozwa faini isiyopungua elfu hamsini(50,000) au isiyozidi laki tano (500,000) au kifungo au vyote kwa pamoja.</p>
---	---	--

BAADHI YA BIASHARA NA VIWANGO VYA ADA YA LESENI KWA MWAKA

NAMBA	AINA YA BIASHARA	ADA OFISI KUU	ADA YA TAWI
1.	Zahanati,/kituo cha afya/maabara	80,000	50,000
2.	Hospitali	150,000	100,000
3.	Madawa muhimu	100,000	80,000
4.	Phamasi	200,000	100,000
5.	Vifaa vya ujenzi	60,000	50,000
6.	Karakana na garage	30,000	30,000
7.	Stationary	20,000	20,000
8.	Duka la nguo	50,000	30,000
9.	Vifaa vya umeme	50,000	25,000
10.	Duka la rejareja	50,000	30,000
11.	Duka la nusu Jumla	200,00	100,000
12.	Kiosk /grocery	40,000	20,000
13.	Mashine za kusaga	30,000	20,000
14.	Mashine ya kukamua mafuta	30,000	20,000
15.	Biashara za mifugo	80,000	40,000
16.	Saluni /vinyozi	20,000	10,000
17.	Maduka ya vilainishi	50,000	50,000
18.	Mitumba rejareja	15,000	10,000
19.	Leseni baada ya kupoteza ya zamani	20,000	10,000
20.	Pombe za kienyeji (komoni , wanzuki, mchujo nk)	30,000	10,000
21.	Pombe za kigeni (bia, konyagi, viloba aina zote)	40,000	
22.	Kuhamisha leseni	10,000	